# Dhanagande na Vichekesho vya Kikabila kama Lugha ya Chuki

*Leonard Chacha Mwita* na *Petra Kanario*
*Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya*

**Ikisiri**

**Nchi ya Kenya ina zaidi ya makabila 42. Wakenya wengi hujitambulisha na jamii zao. Kwa muda sasa, kila jamii imeundiwa dhanagande pamoja na vichekesho vinavyohusiana nayo. Makala haya yanashughulikia uhusiano uliopo baina ya dhanagande, vichekesho vya kikabila, na chuki za kikabila; mada ambayo haijashughulikiwa na watafiti wengi. Aidha, makala haya yanaupima utani huu katika mizani ya sheria za nchi ya Kenya ili kuona kama kuna ukiukaji wowote unaotokana na athari zake. Makala yanaonesha kwamba vichekesho vya kikabila vinavyokiuka mipaka si mzaha tena bali ni namna nyingine ya kueneza chuki. Nadharia zinazotumiwa kuchanganua mada hii ni zile za Majikwezo, Kutopatana kwa mawazo na ile ya Faraja (Raskin, 1985). Nadharia hizi huweza huzingatia madhumuni mbalimbali ya vichekesho. Data ya makala imetolewa kwenye mitandao ya kijamii na pia kutoka kwa kipindi cha Churchill Show. Makala yanaweka wazi changamoto za kisheria katika kukabiliana na hali hii. Pia kunatolewa mapendekezo ya namna ya kukabiliana na hali kama hizi kwa ajili ya utangamano wa kitaifa.**

**Maneno Muhimu:** Dhanagange, Ukabila, Vichekesho, Chuki.

## Utangulizi

Kipera cha vichekesho kimekua sana nchini Kenya tangu miaka ya 1990. Kumekuwepo na watu binafsi na pia makundi mbalimbali ambayo kazi yake imekuwa ni kuwatumbuiza watu kupitia kwa vichekesho. Kikundi ambacho kimetawala kwa muda mrefu ni kile kinachoongozwa na Daniel Ndambuki na huonesha vichekesho vyake kupitia kwa kipindi cha *Churchill Show*. Kumekuwepo na aina mbalimbali za vichekesho nchini Kenya lakini vichekesho vilivyokita katika kabila vimekuwa ndivyo vinavyotumiwa sana na wasanii hawa. Tunapoviangalia vichekesho hivi kwa jicho la juu hatuoni kama vina madhara yoyote lakini tunapoviangalia kwa msingi wa machafuko ya kikabila yaliyotokea nchini Kenya mwaka 2007/2008 na mauaji ya kimbari yaliyofanyika nchini

Rwanda mwaka 1994, tunaanza kufikiria vinginevyo. Mwanzo wa matukio kama haya huwa ni lugha ya chuki ambayo huwaonesha jamii za watu kuwa tofauti na huenda hali hii ikajenga uhasama kati ya makundi hayo. Sura hii inatathmini nafasi ya vichekesho katika utangamano wa kitaifa na kuchunguza kama vinazua chuki miongoni mwa jamii mbalimbali za Kenya.

**Dhana ya Vichekesho vya Kikabila**

Ingawa dhana ya vichekesho vya kikabila imezuka si zamani sana, asili ya kutumia vichekesho kuumbua makundi mengine ya kijamii imekuwepo tangu tamaduni zilipoanza kutagusana (Apte, 1985). Vichekesho vya kikabila ni aina ya vichekesho ambavyo hudhihaki sifa mbalimbali za kikundi cha kijamii na wanachama wake kwa kurejelea misingi yao ya kijamii, kisiasa, kitamaduni, kidini na kiuchumi (Apte, 1985). Hivi ni vichekesho ambavyo vimejikita kwenye tabia, mila, nafsi au sifa zingine za kikundi au wanachama wake kulingana ua utambulisho wao wa kijamii. Vichekesho vingi vya kikabila huonesha kundi husika kama la watu wanaofanya mambo yasiyoeleweka au ya kipumbavu. Kwa namna hii, vichekesho vya kikabila vinatumiwa kuonesha kwamba utamaduni mmoja ni bora kuliko mwingine. Apte (1985) anaendelea kusema kwamba mbali na ile hali yake ya kuburudisha, upo uwezekano wa vichekesho vya kikabila kuficha uovu na nia mbaya na kuendeleza uchokozi usio wa moja kwa moja.

Nchi ya Kenya ina zaidi ya watu milioni 42 ambao wanatoka katika zaidi ya jamii 42. Wakenya wengi hujitambulisha na jamii zao kupitia kwa majina yao ya ukoo, maeneo wanayoishi nchini Kenya, au hata lafudhi zao wanapozungumza Kiswahili au Kiingereza. Kwa kawaida, Mkenya hutambua kabila lake mtu kwa kusikiliza lafudhi yake anapozungumza Kiswahili au Kiingereza. Kwa sababu hiyo, lafudhi imetumiwa kutungia baadhi ya vichekesho vya kikabila.

Pia kuna sifa nyingine zinazotambulisha jamii za watu nchini Kenya kama kile chakula wanachopendelea, wanavyoishi maisha yao, shughuli za kidini, kiuchumi na kitamaduni (Micheka & Muaka, 2006). Wakenya pia wana desturi ambazo zinawaunganisha kwa kuwa zinapatikana katika makabila mbalimbali. Desturi kama hizi humtambulisha Mkenya kwa namna fulani. Matamshi, mitindo, desturi za kitamaduni, na desturi nyinginezo za Wakenya zimepelekea kuwepo kwa utambulisho maalum.

Jinsi watu wanavyochukulia vichekesho hivi huelekezwa na mambo mbalimbali kama utambulisho wa kikabila. Utambulisho wa kikabila ni kiwango ambacho mhusika anaathiriwa na kujitolea kutetea kundi lake. Utambulisho wa kikabila ukiwa wa juu, wanachama wa kikundi watahisi umoja na mshikamano zaidi kati yao. Kikundi kinapokabiliwa na jumbe zinazowadhalilisha kutoka kwa kikundi kingine, basi hakitafurahia jumbe hizo. Lakini wakati ambapo utambulisho wa kikabila ni wa kiwango cha chini, watu hawategemei sana kabila lao na ushikamano wao huwa mdogo. Kwa hiyo, kiwango cha utambulisho wa

kikabila utaathiri namna mhusika anavyochukulia vichekesho vya kikabila vinavyolenga kundi lake.

Ukabila unajidhihirisha nchini Kenya kupitia kwa dhanagande. Dhanagande ni imani kuhusu jamii au kikundi cha watu ambayo inaweza kuwa hasi au chanya. Imani hii hujengwa kwa kuchukua kipengele fulani kuhusu jamii husika na kukikuza kuliko kawaida au kutumia ujumuishaji. Dhanagande ni picha iliyorahisishwa kuhusu mtu au kundi la watu ambalo linashiriki sifa husika zinazorejelewa. Ifahamike kwamba dhanagande huwa ni uwasilishaji usio sahihi wa jamii fulani kwa kutumia kinachofikiriwa kuwa ni sifa wakilishi za wanachama wa kundi hilo la kijamii.

Vichekesho vingi vya kikabla hutumia dhanagande, hasa ile hasi, kama malighafi yake. Matumizi ya dhanagande yanaweza kuwa na matokeo mazuri au mabaya. Aghalabu dhanagande huelekezwa na mielekeo ya watu. Ndonye & Yieke (2015) wanasema kwamba historia ya dhanagande zilizokita kwenye misingi ya kabila zilianza kutumiwa wakati wa ukoloni kama mbinu ya kudhibiti makundi ya kijamii kwa kuhakikisha kuwa jamii hizo zimetengana. Watu wanapoogopa chochote kilicho tofauti wanaishia kutagusana na wale wanaoshiriki nao sifa zinazofanana na hivyo kuendeleza ukabila. Kwa hiyo, dhanagande hufanya watu wakose kuona uzuri wa wingilugha. Msanii anapotoa kichekesho chake kwa kutumia dhanagande hasi kuhusu jamii fulani, watu wanaotoka katika jamii inayorejelewa hawatafurahia kichekesho hicho. Hapa kuna mifano michache ya dhanagande kuhusu jamii mbalimbali nchini Kenya.

1 a) Wajaluo ni watu wenye kiburi na majivuno.

b) Wanawake wote kutoka Nyeri ni hatari.

c) Wakisii wana hasira.

d) Wakikuyu wanapenda pesa.

e) Waluhya wanapenda chakula.

f) Wakamba wanajulikana kwa madawa, ushirikina na eneo kavu wanaloishi.

Hizi dhanagande zimefungamana na vitendo ambavyo vinahusishwa na jamii mbalimbali. Kwa mfano:

2 a) Zungumza kama Mjaluo.

b) Ng’ang’ania bei kama Mkikuyu.

c) Kula kama Mluhya.

d) Ruka kama Mmaasai.

e) Kimbia kama Mkalenjin.

f) Fanya biashara kama Mhindi.

Dhanagande nyingi huwa ni hasi, chache huwa ni chanya. Kwa mfano, Wamaasai walichukuliwa kuwa watu waaminifu ingawa kwa upande mwingine wanaonekana kama watu wasiostaarabika. Aidha, dhanagande inayoeleza Wakikuyu kuwa watu wanaopenda pesa inaweza kutumika kwa njia chanya na hasi pia. Inaweza kutumiwa kueleza kwa nini jamii hii inafanikiwa katika biashara lakini pia inaweza kutumiwa kueleza ni kwa nini watajihusisha na wizi ikiwa pesa zitakosekana. Kwa hiyo, dhanagande hukuza sifa chanya ambazo zinafaidi kikundi lakini pia zinaweza kukuza sifa hasi na hivyo kusambaratisha utangamano wa taifa. Vichekesho kuhusu makundi, yawe ya kijamii, kikazi, kimbari au kitaifa huzingatia sifa mahususi ya kikundi hicho (Gruner, 2000).

## Nadharia za Vichekesho

Kwa mujibu wa Raskin (1985), kuna nadharia tatu kuu za uchanganuzi na uelewa wa vichekesho; majikwezo, kutopatana kwa mawazo na kitulizo/faraja. Nadharia hizi tatu zinachangiana na kukamilishana.

### Nadharia ya Majikwezo (*Superiority Theory*)

Nadharia ya majikwezo huchukulia vichekesho kama njia ambayo kwayo kundi fulani hukejeli na kucheka hali ya kundi la pembezoni. Nadharia hii unahusishwa na dharau, bezo na dhihaka. Carroll (2014) anasema kwamba kicheko hutokana na kutambua udhaifu au kasoro waliyo nayo wengine. Hali hii huliinua kundi moja na kulitweza kundi linalochekwa. Kwa kawaida, vichekesho kama hivi huonesha wanaolengwa kama wapumbavu, mbumbumbu au wasiostahili. Vichekesho hivi huwa kama njia ya kuwadhalilisha wahusika. Kwa namna hiyo basi vichekesho vya kikabila huzingatia kipengele kisicho kizuri katika kundi linalodhihakiwa na wasikilizaji wanacheka ujinga wa kundi hilo, huku wakifurahi kisiri kuwa si wao walio hivyo. Hii ndiyo sababu aina hii ya vichekesho huzalisha kile tunachoweza kuita 'kicheko cha ushindi'. Vichekesho vinapoelekezwa katika kuwaumbua wengine, vinaweza kuwa vya kuchukiza. Hata hivyo, inadhaniwa kwamba vichekesho kama hivi vinaweza kuwa na dhima chanya kama vile kurekebisha tabia mbaya za kijamii. Kumbe tunapocheka tabia mbaya zetu na za watu wengine, hili linaweza kuchangia kurekebisha jamii hiyo iliyopotoka.

Plato alieleza kwamba husuda au wivu ni kipengele cha kimsingi katika vichekesho (Raskin, 1985). Alisema kwamba tunacheka na kufurahia masaibu ya wengine tukiwa tunajua kwamba hatujapatwa na masaibu yaliyowapata. Kwa hiyo, kicheko ni namna ya kuumbua wengine. Kwa jumla, nadharia hii inaonesha mahusiano au mielekeo iliyopo baina ya mzungumzaji na msikilizaji. Hii ni nadharia ambayo inamsafirisha binadamu hadi zamani za kale ambapo mtu alifurahi alipomshinda adui yake katika jambo. Nadharia hii inaona vichekesho kama ushambuliaji wa hadhi ya mtu mwenye nia mbaya.

**Nadharia ya Kutopatana kwa Mawazo (*Incongruity Theory*)**

Nadharia ya pili ni ile ya kutopatana kwa mawazo (incongruity). Nadharia hii inaeleza kuwa vichekesho huwa ni tokeo la utata au njia mbili zisizopatana za kufasiri jambo fulani. Kutopatana kwa mawazo ndio muundo wa kimsingi wa vichekesho ambapo kuna elementi mbili zinazokinzana: inayotarajiwa na isiyotarajiwa. Katika hali hii, hadhira hutarajia jambo fulani lifasiriwe kwa njia A lakini kwa mshtuko inagundua kwamba msimuliaji ameifasiri kwa njia B ambayo haikutarajiwa ingawa ni fasiri inayowezekana na ilikuwapo tangu awali. Matokeo yake yanakuwa ni kicheko. Kwa hiyo, kichekesho husababishwa na kutopatana kwa maelezo yanayotarajiwa na matokeo yasiyotarajiwa. Muundo wa kichekesho hukiuka ruwaza za fikra na matarajio yake. Msimuliaji huifanya hadhira itarajie jambo fulani lakini ghafla anachukua mwelekeo ambao haukuwa unatarajiwa. Hili ndilo hutekenya akili ya msikilizaji na kusababisha kicheko pale msikilizaji anapogundua kwamba alikosa kuelewa fasiri mbili zilizo katika kauli kutoka mwanzo wa masimulizi. Nadharia hii inaeleza kwamba katika kichekesho tunaelekezwa kushikilia mkondo fulani wa fikra hadi pale ghafula tunapoondolewa kwenye mkondo huo na kuingizwa kwa mwingine ambao hatukuwa tunautarajia.

Attardo & Raskin (1991) wanadai kwamba kichekesho huwa na mwanzo unaojenga msingi kwa maelezo kisha kuna kipeo (punchline) ambacho husababisha mabadiliko kutoka kwa maelezo A hadi B kwa kumfanya msikilizaji ashtuke kwa kugundua kwamba kulikuwa na namna tofauti ya kufasiri maelezo aliyopewa tangu mwanzo. Kwa hiyo, kipengele cha mshangao au mshtuko ni muhimu sana katika nadharia hii. Kipengele hicho cha mshtuko huwasilishwa na kipeo cha kichekesho. Nadharia hii inahusu matumizi ya lugha, hususan utata katika lugha. Huu ni uwezo wa kuona ufanano kati ya vitu viwili tofauti (Raskin, 1985).

Nadharia hii ya kutopatana kwa mawazo ndiyo hutumiwa sana na wachekeshaji hasa wale wanaotunga vichekesho visivyo vya kikabila. Hapa kuna mfano:

> 3) Nilimwona mwanamke mmoja, huku mbele (anaonesha kifua) alikuwa na mati…(material) na kule nyuma (anaonesha makalio) alikuwa na mata…(matatizo).

Msanii wa kichekesho hiki alikuwa anataja silabi mbili za mwanzo za maneno nyeti katika kichekesho hiki na kuwaachia watu wakamilishe. Kwa kuwa wasikilizaji walikuwa wamepata maelezo ya mwanzo ya kichekesho walitaja ‘matiti’ na ‘matako’ ili kukamilisha maneno ambayo hayakuwa yamekamilika. Hata hivyo, wasikilizaji waligundua kwamba msimuliaji alikuwa amewaelekeza kwenye mkondo fulani wa fikra na mara moja akawaacha hapo na kutoa majibu tofauti. Hili ndilo linalosababisha kicheko.

Mfano wa pili umetolewa na Raskin (1985: 32):

> 4) "Je, daktari yupo nyumbani?" mgonjwa wa bronkitisi aliuliza kwa mnong'ono. "Hapana," mkewe daktari ambaye ni mrembo chipukizi akajibu kwa kunong'ona. "Pita ndani haraka."

Katika kisa hiki, ni wazi kuwa mgonjwa anataka kumwona daktari ili amtibu. Mgonjwa ananong'ona kwa sababu ya ugonjwa wake. Anapoalikwa kuingia ndani wakati daktari hayupo tunaona mkinzano wa aina fulani. Hali kwamba mke wa daktari ni mrembo chipukizi inakuwa mwanzo wa fasiri nyingine kujitokeza. Mke wa daktari anaponong'ona na kumwambia mgonjwa aingie ndani haraka basi tunajua kwamba yeye anafikiri kuhusu uasherati. Tangu mwanzo mke wa daktari alifasiri kuwa bwana huyu alinong'ona kwa kuwa alikuwa na kusudi la uasherati; hakuelewa kwamba alifanya hivyo kwa sababu ya ugonjwa. Kicheko kitatokea hapa baada ya kugundua jinsi hivi vitu viwili visivyohusiana vililetwa pamoja.

**Nadharia ya Tulizo (*Release Theory*)**

Nadharia ya tulizo inahusishwa na Sigmund Freud na Herbert Spencer. Nadharia hii inaeleza kwamba vichekesho husababisha faraja. Wasanii hutunga vichekesho ambavyo vinalenga udhaifu wao, kama namna ya kujiachia huru. Kicheko kinapotokea kinamwezesha mhusika kuachilia nguvu zenye wahaka au fadhaa zilizokuwa zimefungiwa mwilini mwake na matokeo yake ni faraja na utulivu mwilini. Vicheko hutuweka huru kutokana na minyororo ya mifumo ya kiutambuzi, kikaida, kimantiki, kiisimu, na kimaadili. Mambo mengi yanayomfanya binadamu acheke ni yale ambayo anajua kwamba hayana chembe ya ukweli, na ambayo yangekuwa kweli tu katika ndoto. Jambo au tendo linalokiuka kaida humpa binadamu uhuru kutoka kwa mikatale ya maisha. Kwa hiyo watu kama hawa huwa wanajicheka wenyewe. Huu ni mtazamo wa zamani sana wa kueleza vichekesho na hautumiwi sana siku hizi.

Kwa kurejelea nadharia hizi tatu kuu za vichekesho, tuna hakika kwamba vichekesho hutumiwa kumkuza mtu au kundi la watu dhidi ya wengine, kuondoa fadhaiko, au kuonesha kutopatana kati ya mawazo mawili. Sura hii imezingatia zaidi nadharia ya majikwezo na nadharia ya tulizo au faraja.

**Mbinu za Utafiti**

Data imetolewa kwenye mitandao ya kijamii ambapo waandishi walipitia maandishi yanayohusu vichekesho. Pia data ilikusanywa kutoka kwa kipindi cha *Churchill Show Live*. Kipindi hiki hupeperushwa katika runinga ya NTV katika awamu mbili kuu. Awamu ya kwanza ni ile ya *Churchill Show Live* ambayo huoneshwa Jumapili saa mbili hadi saa tatu usiku. Awamu ya pili huitwa *Churchill Raw* na hupeperushwa siku ya Alhamisi kuanzia saa mbili u nusu hadi saa tatu usiku. Baadhi ya vipindi hivi vilitazamwa moja kwa moja kutoka kwenye

televisheni viliporushwa hewani lakini vingine vilitazamwa kutoka kwa YouTube. Vichekesho hivi vilitolewa kwa Kiingereza, Kiswahili, Sheng au hata kwa kuchanganya lugha. Kwa hiyo, ilibidi waandishi wa makala haya watafsiri baadhi ya vichekesho kwa Kiswahili. Mwisho, kuna vichekesho ambavyo vilikusanywa kutoka kwa gazeti la *Daily Nation*.

**Lugha ya Chuki**

Kama ilivyoelezwa katika utangulizi, makala haya yanachunguza vichekesho vinavyochota maudhui yake kutoka kwa tabia za jamii mbalimbali nchini Kenya ili kuona kama vinatumika kusambaza chuki. Ili kuweza kushughulikia jambo hili vyema, itabidi tueleze chuki ni nini na sheria zinazohusiana na suala hilo nchini Kenya. Tutachukulia 'lugha ya chuki' kuwa mifumo yote ya kujieleza ambayo inasambaza, kuchochea, kuendeleza au kuhalalisha chuki, ubaguzi, vitisho, matusi, kutovumilia, na uhasama dhidi ya watu wengine (Kimotho & Nyaga, 2016). Lugha ya chuki hurejelea maneno ya uchochezi na chuki dhidi ya watu wengine kwa sababu ya kujitambulisha kwao na kundi mojawapo la kijamii. Inaonekana kwamba lugha ya chuki huelekezwa kwa mtu au kundi la watu ambao wanafikiriwa kuwa duni kwa misingi ya sifa fulani inayojenga utambulisho wao kama mbari, kabila, jinsia, utaifa na kadhalika. Lugha ya chuki inarejelea tabia za binadamu za kimawasiliano zinazohusu matumizi ya maneno au ishara ambazo zinaonyesha uhasama au chuki dhidi ya watu binafsi au kundi la watu kwa misingi ya kuwa wanachama wa kikundi fulani. Ni dhahiri kwamba ni vigumu kutambua lugha ya chuki moja kwa moja kwa sababu si lazima ijitokeze katika mawasiliano yaliyojaa mihemko ya kihisia, inaweza pia kujitokeza katika taarifa zinazoonekana kuwa razini.

**Jinsi Sheria za Kenya zinavyoshughulikia Lugha ya Chuki**

Changamoto kubwa iliyopo katika nchi ya Kenya inahusu utangamano wa kitaifa. Kumekuwepo na desturi za Wakenya kulipa kila suala mtazamo wa kikabila. Kwa hiyo, lugha ya chuki imetanda sana katika jamii za Kenya. Matumizi ya lugha inayodhalilisha jamii fulani yameonekana hasa katika malumbano ya kisiasa tangu miaka ya 1990. Ni kutokana na hali hii ambapo matumizi ya lugha ya chuki na dhanagande hasi yamesambaa sana. Kwa hiyo, suala hili limekitwa katika sheria za nchi ili kuwalinda watu binafsi na makundi ya kijamii. Chombo kimoja ambacho kiliundwa ili kushughulikia lugha ya chuki ni Tume ya Uwiano na Utangamano. Kazi yake hasa ni kuwezesha na kuendeleza mahusiano mazuri, umoja na amani baina ya watu wa jamii mbalimbali nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Onyoyo (2012), Sheria ya Tume ya Uwiano na Utangamano Nambari 20 ya mwaka 2008 katika Ibara ya 13 inafafanua lugha ya chuki kama:

(a) matumizi ya lugha au tabia ya kutisha, kutukana, au kuonesha maandishi kama hayo;

(b) kuchapisha au kusambaza matini zilizoandikwa;

(c) kuwasilisha au kuongoza kadamnasi mchezo wa kuigiza;

(d) kusambaza, kuonesha au kucheza picha; au

(e) kutoa au kuendesha programu ambayo inatisha, inatukana au inahusu matumizi ya maneno ya kutisha, au tabia kama hizo ikiwa mtu huyo ana nia ya kuchochea chuki za kikabila, au kwa kuzingatia muktadha husika, kuna uwezekano wa kuchochea chuki za kikabila.

(2) Mtu yeyote atakayevunja sheria, kwa mujibu wa ibara hii, atapigwa faini ya shilingi zisizozidi milioni moja au atafungwa kwa muda usiozidi miaka mitatu au zote mbili.

(3) Katika ibara hii, "chuki za kikabila' humaanisha chuki dhidi ya kundi la watu wanaobainishwa kwa rangi, mbari, taifa (pamoja na uraia) au kabila au misingi ya kikabila.

Ingawa tume hii ina sheria dhidi ya lugha ya chuki inahitaji vyombo vya Dola kama polisi kusaidia kuitekeleza. Tume hii imekuwa ikishughulikia hili swala la lugha ya chuki na uchochezi wa kikabila ingawa mafanikio hayajakuwa makubwa sana.

Lugha ya chuki pia imeshughulikiwa katika Sheria ya Vyombo vya Habari ya 2013, sehemu yenye anwani "Kanuni za Maadili za Desturi za Uanahabari Nchini Kenya", Kanuni ya 26 ambayo inaeleza kwamba:

> Epuka kunukuu watu wanaotoa kauli za kuaibisha kwa misingi ya kabila, mbari, dini, rangi na jinsia. Maneno yanayobagua watu kimbari au yaliyo hasi yanastahili kuepukwa.

Sheria hii inadhibiti utendakazi wa wanahabari na kuwaelekeza kuepuka kuchangia usambazaji wa lugha ya chuki. Kwa kweli, sheria hii ya vyombo vya habari inatoa maadili ya kikazi ambayo wanahabari wanatakiwa kufuata. Sheria hii inaelekeza wanahabari kuwa makini kuhusu yale wanayoripoti ili yasiwe mambo ambayo yamesheheni lugha ya chuki na yanaweza kuwachochea watu.

Chombo kingine kinachotumiwa kudhibiti lugha ya chuki ni Katiba ya Kenya 2010. Kuna ibara kadha wa kadha ambazo zinazungumzia usawa dhidi ya kubaguliwa. Ibara hizo ni:

Ibara 27(1) inamhakikishia kila mtu ulinzi sawa. Inasema: "Kila mtu yu sawa mbele ya sheria na ana haki ya kulindwa na kupata manufaa sawa ya sheria."

Ibara 27(2) inasema: "Usawa unajumuisha kupata haki na uhuru wote wa kimsingi kwa njia iliyo kamili na sawa."

Katika kufasiri sheria hizi kwa mujibu wa mada ya vichekesho vya kikabila, tunaona kwamba ikiwa lugha ya chuki italenga kundi moja au sehemu ya jamii, athari zake kama vile vurugu au madhara yoyote yatakayotokea dhidi ya kundi hilo kutokana na lugha ya chuki yatakuwa yanakiuka haki za kundi hilo. Kwa

hivyo kikundi kilichoathiriwa hakiwezi kufurahia kikamilifu uhuru unaotolewa katika katiba ya nchi.

Ibara ya 27(4) inaeleza kuwa: "Serikali, kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, haitakuwa na ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa misingi yoyote ikiwemo mbari …asili ya kikabila na kijamii …dini, dhamiri, imani, utamaduni, mavazi, lugha au kuzaliwa."

Ibara hii inaipa serikali jukumu la kutopendelea dhidi ya sehemu yoyote ya jamii. Pia ibara hii inawalinda wananchi dhidi ya lugha ya chuki inayoweza kuendeshwa na mawakala wa serikali.

Ibara ya 27(5) inaeleza kuwa: "Mtu hatakuwa na ubaguzi dhidi ya mwingine kwa njia ya moja kwa moja au vinginevyo katika misingi iliyotajwa na kuoneshwa na ibara ya (4)."

Katiba ya Kenya 2010 inafahamika kwa kuwapa wananchi uhuru wa kujieleza na wa ubunifu wa kisanii. Hata hivyo, Ibara 33(1) inaeleza kuwa uhuru huu una mipaka. Inasema: "Haki ya uhuru wa kujieleza haiambatani na:- (a) propaganda ya vita; (b) uchochezi wa ghasia; (c) hotuba za chuki; au (d) utetezi wa chuki…"

Ibara ya 77(3) ya Kanuni ya Adhabu (Penal Code) pia inazungumzia lugha ya chuki. Inaeleza hivi:

> (1) Mtu yeyote ambaye anajaribu kufanya au anajitayarisha, au anakula njama na mtu mwingine kufanya kitendo kilicho na kusudi la kiuchochezi, au anayetamka maneno yoyote akiwa na kusudi la kuchochea, ana hatia na anastahili kufungwa kwa muda usiozidi miaka mitatu…
>
> (3) Kwa madhumuni ya ibara hii, 'uchochezi' unamaanisha… (e) iliyo na kusudi au inayoazimia kuchochea hisia za chuki baina ya mbari au jamii mbalimbali nchini Kenya: Mradi tu yaliyomo katika aya hii hayatahusisha maoni au ukosoaji unaotolewa kwa nia njema na ulio na kusudi la kuondoa vyanzo vyovyote vya chuki au uadui baina ya mbari au jamii.

Aidha, Kanuni ya Adhabu inazo sheria ambazo zinahusu uchochezi unaosababisha vurugu na ukiukaji wa sheria. Ibara ya 96 ya Kanuni ya Adhabu inaeleza kuwa "Mtu yeyote ambaye, bila sababu ya kisheria, anao wajibu wa kuthibitisha, anatamka, kuchapisha maneno yoyote, au anatenda kitendo chochote, kinachoonyesha au kuashiria kwamba ana nia ya kutenda, au kutotenda, kitendo chochote anbacho kina kusudi la:

i. kusababisha kifo au madhara kwa mtu yeyote au mkusanyiko, jamii au kikundi cha watu; au
ii. kupelekea kuwepo kwa madhara au uharibifu wa mali; au

iii. kuzuia au kushinda kwa vurugu au kwa njia nyingine zisizo za kisheria utekelezaji wa sheria yoyote iliyoandikwa au kusababisha kukaidi au kutotii sheria yoyote kama hiyo, au ya mamlaka yoyote halali, ana hatia na anastahili kifungo cha muda usiopungua miaka mitano"

Sheria hizi zote zinamtetea mwananchi dhidi ya ubaguzi na dhuluma za aina yoyote na zinasaidia kupunguza matumizi ya lugha ya chuki. Kilicho wazi ni kwamba nchi ya Kenya haina ukosefu wa sheria ambazo zinaweza kutumiwa kudhibiti lugha ya chuki. Suala la kubaini kama vichekesho vya kikabila hutumia lugha ya chuki limeshughulikiwa katika sehemu inayofuata.

## Vichekesho na Lugha ya Chuki

Ndonye, Yieke & Onyango (2015) wanaeleza kuwa tafiti zilizofanywa zinaonesha kwamba vichekesho vyenye misingi ya kikabila ni mfano wa sime yenye makali pande zote mbili; wakati fulani vinaweza vikaudhi na wakati mwingine vinaburudisha. Matumizi ya dhanagande kuirejelea jamii fulani ya watu kunaweza kuwa na kusudi tu la kuchekesha na huenda haitazingatiwa sana na wasikilizaji wa vichekesho. Hata hivyo, kuna wakati dhanagande hizi zitaaminiwa na kutumiwa katika hali zisizo za mzaha. Tunafahamu kwamba Wakenya wengi hucheka na kufurahi wanaposikiliza vichekesho hivi. Lakini je kuna athari yoyote ya dhanagande ambazo wasanii hawa hurudiarudia katika maonyesho yao kuhusu zaidi ya makabila 42 yaliyo nchini Kenya? Dhanagande na vichekesho vilivyokita katika kabila huweza kuwa mbegu ya kukuza utofauti na chuki. Anastasia (2016) anasema kwamba ingawa vichekesho haviwezi kupigwa marufuku, heri tufahamu kwamba vina madhara yake. Matumizi na usisitizaji wa dhanagande huwafanya watu kukosa kuona uzuri wa uanuwai. Woga wa kilicho tofauti huhakikisha kwamba mtagusano unatokea tu kati ya watu walio na utamaduni mmoja. Hili huimarisha ukabila au ubaguzi kwa misingi mbalimbali. Mwishowe utangamano na uanuwai hukwazwa.

Suala la kabila limekuwa maudhui muhimu katika vichekesho hasa kwenye kipindi cha *Churchill Show Live*. Wachekeshaji wengi katika onyesho hili hutunga vichekesho vyao kwa kutumia dhanagande kuhusu jamii mbalimbali nchini Kenya. Baadhi ya jamii ambazo zilirejelewa katika vichekesho tulivyokusanya ni Wakikuyu, Wakalenjin, Waluo, Wakamba, Wamaasai, Wasomali, Wakisii na Wahindi. Katika sehemu hii inayofuata tutatoa na kuchanganua mifano ya vichekesho hivyo ambavyo asili yake ni dhanagande za baadhi ya jamii hizi.

### Dhanagande 1: Waluhya wanapenda chakula

Kutokana na dhanagande hii, kuna vichekesho vingi ambavyo vimejitokeza. Hapa kuna mifano:

5a) Mbali na kuku, Waluhya wanapenda ndege 'zingine' kama helikopta (Murabula, 2015).

b) Nimefungua Biblia ya Mluhya, kupitia *New Testament*, sioni *verse ya Jesus feeds 5000 people with 5 loaves and 2 fish* (Murabula, 2015).

c) Eti ukila ugali wiki tatu mfululizo, wiki ya nne *accent* ya Kiluhya inajileta yenyewe (Murabula, 2015).

d) Uko kwa *Club* unacheza kuku *dance*… kidogo kidogo Mluhya anakuuma mgongo (Murabula, 2015).

e) *Blessings come double double* wakati Mluhya anafukuza kuku halafu itoroke iingie *posho mill* (Murabula, 2015).

f) Una*visit* mtu halafu 3 *days consecutive* hajapika ugali, si*complain*, nashangaa tutakaa njaa siku ngapi (Murabula, 2015).

g) "Usiwahi *interrupt* Mluhya akiwa kwa mkutano. Mluhya akiwa kwa mkutano ajenda huwa ni ugali na A.O.B huwa ni mboga" (Churchill Show Live, Season 03 Episode 53).

Vichekesho vilivyotolewa katika (5) vinaendeleza dhana kwamba Waluhya wanapenda chakula, hususan ugali na nyama ya kuku. Ingawa tunaweza kusema kwamba baadhi ya vichekesho hivi vina ubunifu, havitoi taswira kamili ya jamii inayozungumziwa. Vitawachekesha baadhi ya watu lakini wengine watahisi kwamba jamii yao inakosewa heshima. Si kweli kwamba Waluhya wanapenda chakula kuliko jamii zingine, lakini huu ni ujumlishaji ambao umenata na unatumiwa kuipambanua jamii hiyo. Jinsi vichekesho hivi vilivyo hatuwezi kusema kwamba lugha ya chuki imetumiwa lakini vinaweza kuwa ndiyo mbegu ya utengano wa jamii.

Billig (2001) amesema kwamba huenda kuna uhusiano wa chini kwa chini baina ya vichekesho kama hivi na fikra za kupendelea upande mmoja. Vichekesho hivi vinafasiriwa vyema na nadharia ya majikwezo ambapo anayetoa kichekesho na wanaovifurahia wanacheka kwa kufahamu kwamba si wao wanaodhalilishwa. Hivi basi ni vichekesho vya kuumbua au kushushia hadhi kikundi kingine. Anayetoa kichekesho anakuwa kama anayesema kwamba hali anayoifahamu kuwa mwafaka ni ile iliyo kinyume na kilicho katika kichekesho hicho.

**Dhanagande 2: Wakikuyu wanapenda pesa**

Kutokana na dhanagande hii imechukuliwa kwamba Wakikuyu ni wezi kwa sababu watafanya lolote ili kuzipata pesa lakini pia imechukuliwa kwamba jamii hii hufanya bidii sana ili kupata pesa. Ifuatayo ni mifano ya vichekesho ambavyo vilikusanywa:

6 a) Yesu alisulubiwa na wezi wawili. Angejaribu kutumia wazee wa Kiambu hatungekuwa na *Easter*. Wazee hawa wawili wangekuwa wezi wangesema hivi:

Nderitu: Kama wewe ni mwana wa Mungu, ukienda mbinguni unikumbuke.

Kinuthia: Tukumbukaneni hapa kabla twende mbinguni, mnajua tumelalia pesa. Hii misalaba ni *hardwood*. Tuokoe tuiuze (Season 05 Episode 47).

b) Kwa Wajaluo, pesa si shida; kwa Wakikuyu si kila kitu, ndicho kitu pekee.

c) Msichangae kwa nini nimefaa hifi led… mwarimu hayuko aloud…

Kichekesho cha 6c) kinahusu lahaja ya Nyeri ya Kikuyu inayojulikana kwa kuchanganya sauti /r/ na /l/. Kwa hiyo, mchekeshaji anatumia matamshi hayo ya Kiswahili ili kuwadhihaki wazungumzaji kutoka Mkoa wa Kati nchini Kenya. Kichekesho hiki kilitolewa na mchekeshaji aliye na lakabu ya Teacher Wanjiru. Hapa ni kana kwamba anaikejeli jamii yake. Huu ni mfano wa watu kujicheka wenyewe, kicheko kinacholeta faraja.

Kimotho na Nyaga (2015) walifanya utafiti kupeleleza athari za chuki za kikablia zinazosambazwa kupitia mitandao ya kijamii. Utafiti huu ulichunguza wanafunzi kutoka vyuo vikuu vinne nchini Kenya na matokeo yalikuwa kwamba 50% ya wahojiwa walisema kuwa walihisi vibaya waliposoma maandishi yenye lugha ya chuki iliyoelekezwa kwa kabila lao. Ni wazi basi kwamba ijapokuwa vichekesho vyenye misingi ya kikabila huchekesha, pia vinakera jamii inayodhalilishwa.

**Dhanagande 3: Wajaluo ni watu wenye kiburi na majivuno**

Wajaluo ni watu ambao husawiriwa kuwa wenye kiburi kingi. Kwa hiyo, ucheshi hutolewa kuonesha jinsi kiburi chao kinavyodhihirika. Angalia vichekesho vilivyo katika mfano namba 7.

7 a) Kwa Wajaluo, pesa si shida; shida ni namna ya kuzitumia. Msanii mmoja alisema, "Ukipata Mjaluo analia, huyo hana shida bali ana milioni 50 na ameshindwa jinsi ya kuzitumia." Ukimwuliza anachokililia atakujibu, "Nina biashara hamsini na nne, nimewachangia mayatima, nimechangia kanisa ambalo hata mimi sishiriki." (Churchill Show, Season 3 Episode 54).

b) Ukipata Mjaluo analalamika jua kwamba huyo anaringa tu. Mzee mmoja aliona ndege ikipita hewani akasema "Wazee, naomba mkamshauri mtoto wangu Otunga, huyu kijana anandesha ndege vibaya sana, umeona jinsi alivyopita na madharau hata bila kumsalimia baba yake?" (Churchill Show, Season 3 Episode 54).

c) Ukienda Luo Nyanza utashangaa kukuta Range Rover karibu na nyumba ya nyasi. Ukiuliza mwenyewe anakwambia ile nyumba ya nyasi ni *kitchen, bedroom* ni Range Rover. (Chanzo: Mtandao)

d) Ujaluo ni gharama. Adamu angekuwa Mjaluo, angemuuliza Mungu: Mungu yawa, hata kama wewe ndiye muumbaji, lazima uniumbe kwa kutumia udongo. (Chanzo: Mtandao)

Vichekesho 7a na c) vinatoa ujumbe kwamba Wajaluo ni wabadhirifu na hawajui kuwekeza. Pesa zote wanazopata wanazitumia kwa starehe. Aidha, kichekesho 7c) kinatoa ujumbe kwamba kuna uchochole mwingi katika jamii hii. Bila shaka, kichekesho hiki kitawatekenya watu wa jamii nyingine lakini watu wa jamii hii wataghadhabishwa na hata kuwachukia watu wa jamii nyingine wanaowalenga na mizaha hiyo.

**Dhanagande 4: Wakamba wanajulikana kwa ushirikina na kuishi eneo lenye ukame**

8 a) Watu wanasema maji ni uhai lakini leo nimekuja ukambani nikajua jua ndilo uhai. (Churchill Kitui Edition, Season 07 Episode 42)

b) Watu husema Ukambani hakuna maji, nikija nimeona *car wash*, kwani wanaosha magari kwa bia? (Churchill Kitui Edition, Season 07 Episode 42)

c) Eti Wakamba wanaweza kutengeneza sambusa ya maji. (Chanzo: Mtandao wa Facebook)

d) Eti Mkamba akikojoa zaidi ya mara mbili kwa siku, hiyo ni *showoff*. (Chanzo: Mtandao wa Facebook)

e) "Kwa nini mlilipa ada ya kiingilio, nilidhani mtakoroga maji kwa beseni kisha mtazame kutoka nyumbani" (Churchill Kitui Edition, Season 07 Episode 42).

Vichekesho hivi (8a, b na c) vinarejelea tabianchi ya Ukambani kuwatania wenyeji wa Kitui kuhusu hali ngumu waliyo nayo. Jua ni kali na maji hayapatkani kwa urahisi. Kichekesho cha 8e) kinahusu uchawi na ushirikina wa jamii iliyotajwa. Kinachodhihirika kutokana na mifano ya vichekesho vilivyokita katika dhanagande vilivyotolewa katika sehemu hii ni kwamba ingawa vinachekesha, vinawatenga watu pia. Vichekesho hivi huchekesha kila mtu mara ya kwanza vinaposimuliwa, baada ya hapo vinaudhi baadhi ya watu. Wale ambao jamii zao zinalengwa na vichekesho hivyo huhisi kwamba wanashambuliwa na kutengwa. Hapa ndipo tatizo la vichekesho kama hivi huanzia kwa kurejelea kile kinachochukuliwa kuwa tabia za kundi hilo zisizostahili. Kwa hiyo, kuwepo kwa dhanagande si tatizo, bali tatizo ni kuzitumia dhanagande hizo kwa njia mbaya. Pia ifahamike kwamba wachekeshaji wanapotoa vichekesho vya kikabila huwa wanatumia vichekesho kama barakoa wanamojificha na kuzungumzia mawazo ambayo kwa kawaida hayangekubalika katika mawasiliano. Kisaikolojia, vichekesho kama hivi huleta suala la unyanyapaa ambapo jamii fulani zinakejeliwa kwa vitendo vyao, wanakotoka na kadhalika. Vichekesho hivi

vinakuza upendeleo, tathmini na mielekeo hasi na hata ubaguzi. Hili huenda likazua hisia za aibu, kutengwa na chuki kwa kundi linalolengwa. Vichekesho kama hivi huenda visiwe na athari ya moja kwa moja vinapotolewa lakini dhanagande hizi kuhusu jamii mbalimbali huhifadhiwa akilini na huweza kutumiwa baadaye, kwa mfano na wanasiasa wenye nia mbaya kama ilivyofanyika nchini Kenya miaka 2007/2008, kukejeli na kutusi jamii hizo nyingine. Tatizo linapotokea baina ya jamii mbili, dhanagande zinakuwa msingi wa tofauti za jamii hizo na zinakuwa mbegu ya kupanda chuki baina ya makundi hayo. Pia, kuna watazamaji wa *Churchill Show* ambao huchukulia kwamba kile wanachosikia kuhusu dhanagande ni ukweli mtupu. Watu kama hawa hupata picha potovu kuhusu jamii zinazosimuliwa katika vichekesho.

Suala muhimu la kufikiria ni kama vichekesho hivi vinakiuka sheria za nchi kwa kutumia lugha ya chuki. Hadi hapa imebainika kwamba jinsi vichekesho hivi vinavyoendeshwa havikiuki sheria za nchi. Hata hivyo, dhanagande zinazotumiwa katika vichekesho hivi huwa mbegu ya uhasama baina ya jamii. Kwa mfano, mfanyabiashara mmoja wa kike katika Soko la Wakulima Nairobi alipoteza kibeti chake akasema, "Shida ya hii soko ni kwamba Wakikuyu ni wengi sana. Sijui tutawafanyaje?" (USAID, 2011: 47). Kauli hii inazingatia dhanagande kwamba Wakikuyu ni wezi. Hali inapoanza kuwa hivi inatoka kwenye vichekesho na kuwa suala zito linaloweza kuzusha uhasama kwa urahisi. Tunajua kwamba kutokana na dhanagande hizi, kumekuwepo na matusi mengi mtandaoni kwa msingi huo. Mara tu mazingira ya chuki yanapojitokeza, yanaweza kusababisha msururu wa uhalifu wa chuki. Ni muhimu kufahamu kwamba taarifa haiwi uhalifu wa chuki isipokuwa ikiwa inasababisha chuki, inaifanya jamii moja kuonekana duni, inasababisha kikundi au jamii kudharauliwa, inashusha hadhi au kuvunjia heshima jamii moja mbele ya nyingine, au inadhalilisha kikundi au jamii (USAID, 2011). Kitu kilicho kigumu kuthibitisha katika vichekesho hivi ni kama msanii alikuwa na nia ya kuchekesha tu au alikusudia kuchochea na kutweza jamii moja.

## Hitimisho

Sura hii imejadili vichekesho vyenye misingi ya kikabila na kutoa tathmini kama vinafaa kuwekwa kwenye kategoria ya lugha ya chuki. Vichekesho hivi hujengwa kwa kutumia dhanagande kuhusu jamii mbalimbali. Imebainika kwamba vichekesho hivi havikiuki sheria yoyote nchini Kenya. Hata hivyo imeonekana kwamba vinapanda mbegu ya uhasama inayoweza kutumiwa jamii mbili zikitofautiana. Imeelezwa kwamba dhanagande zinaweza kutumiwa kama matusi na huwa chanzo cha kugawika na kujitofautisha kwa watu katika nchi. Machafuko yaliyotokea nchini Kenya mwaka 2007/2008 ni mfano wa tukio linaloweza kutokea. Inapendekezwa kwamba wasanii washauriwe kutoa vichekezo visivyokita katika dhanagande za kikabila ili kuendeleza utangamano katika jamii.

## Marejeleo

Apte, M .L. *(1985). Humour and Laughter: An Anthropological Approach*. Ithaca and London: Cornell University Press.

Attardo, S., & Raskin, V. (1991). Script theory revis(it)ed: Joke similarity and joke representation model. *Humor: International Journal of Humor Research, 4*(3-4), 293-347.

Billig, M. (2001). Humour and Hatred: the Racist Jokes of the Ku Klux Klan. *Discourse and Society*, 12(3): 267 – 289.

Carroll, N. (2014). *Humour: A Very Short Introduction.* Oxford: Oxford University Press.

Gruner, C. R. (2000). *The Game of Humor*. New Brunswick: Transaction Publishers.

Kimotho, S. G. & Nyaga, R. N. (2016). Digitized Ethnic Hate Speech: Understanding Effects of Digital Media Hate Peech on Citizen Journalism in Kenya. *Advances in Language and Literary Studies* Vol. 7, No. 3, 189 – 200. Australia: Australian International Academic Centre.

Michieka, M. & Muaka, L. (2016). Humor in Kenyan Comedy. In Doris L. Payne, Sara

Pacchiarotti & Mokaya Bosire (eds.), *Diversity in African Languages*, 559–576. Berlin: Language Science Press.

Murabula, C. (2015, June 15). The Demons of Hate Speech are Laughing at our Jokes. *Daily Nation*

National Cohesion and Integration Act No. 12 of 2008. National Council for Law Reporting.

Ndonye, M., Yieke, F., & Onyango, J. O. (2015). Ethnicity as Discursive Construct in Kenyan Television Comedy: Humorous Harm? *The Journal of Pan African Studies* (JPAS) Vol. 2, No. 8, pp. 44-60.

Onyoyo, P. O. (2012). Criminality in Hate Speech Provision in the Laws of Kenya – Jurispudential Challenges. In Herz, M. & Molner, P. (eds.), *The Content and Context of Hate Speech:Rethinking Regulations and Responses,* Cambridge: Cambridge University Press.

Raskin, V. (1985). *Semantic Mechanisms of Humor*. Dordrecht: D. Reidel Publishing Company.

USAID (2011). *Police Training Manual on Enforcing the Law of Hate Speech*. Nairobi: National Cohesion and Integration Commission.